# “TEGA SIKIO UJIFUNZE ELIMU YA KAWAIDA”

**<u>Rekodi za Wanyama – Kukimbia, kuruka na kadhalika</u>**

Mwandishi-Leona Frommelt
Mwelekezi- Maja Dreyer

## <u>Wahusika</u>

Mtangazaji
Jenny- Msichana (14)
Jack - Mvulana (15)

## <u>Sehemu</u>

Barabarani
Nyumbani kwa Jack
Uwanjani

**<u>Sauti</u>**

Barabarani, magari
Watu wakitembea, minongono
Mikebe ya maji ikigongana
Watu wakicheza

**Mtangazaji:**

Hujambo na karibu kwa mfululizo wa mchezo wetu Tega sikio ujifune. Jenny na Jack wanakutana tena--- na kuendelea na shindano lao la kupimana ujuzi. Lakini leo mambo ni tofauti. Jenny haamini macho yake anapomuona Jack akitokwa na jasho. Jack ambaye si kawaida yake ya kufanya mazoezi sasa imekuwa desturi kana kwamba anajiandaa kwa michezo ya Olimpiki.Jambo hili limemshangaza sana Jenny. …Mara ghafla wawili hao waanza kutafakari ni mnyama gani anayeweza kukimbia kwa kasi au kuruka zaidi. Karibu

## Sura ya Kwanza : Jenny akutana na Jack ambaye anafanya <u>mazoezi ya kukimbia barabarani.</u>

*Sauti za barabarani.*

**Jack**: *(akisikika anahema*) Habari Jenny!

**Jenny:** *(kwa mshangao):* Mzuri Jack, vipi? Unahema sana! Usiniambie kuwa siku hizi wewe ni mwana michezo.

**Jack***: ( akiwa angali anahema)*: Ndio mimi ni mwana-michezo. Niko mazoezini. Kwani unashangaza.?

**Jenny:** Kwa wewe – ndio ni jambo la kushangaza. Unajua kawaida yako ni kukaa kitako tu bila kufanya lolote.

**Jack:** Siku hizo zilikwisha! Sasa mimi ni mwana michezo

**Jenny:** *(Na sauti ya kutoamini):* Wewe? Mkimbiaji kweli! Usinichekeshe, wajua nisikia hivyo naona kama utani tu

**Jack:** Utani?

**Jenny:** Yule konokono aliyemkalia Kasa alisema nini?

**Jack:** Sijui!.

**Jenny:** "Taratibu mwenzangu , usiwe na pupa!"

**Jack:** Wachekesha kweli, Jenny. Utashangaa. Ikiwa nitaendelea kufanya mazoezi hivi, nitashinda nishani ya dhahabu katika mbio za mita mia moja. Hapo ndipo utaacha kunilinganisha na konokono au kasa, bali, aaa ee *(Jack anafikiria)* yule mnyama anayekimbia kwa kasi zaidi duniani.

**Jenny:** Mnyama gani huyo?

**Jack:** Sijui lakini nitauliza. Hata hivyo napaswa kuendelea na mazoezi.

**Jenny:** *( akimgeukia huku akimwambia):* Sawa basi. Wakati tutakapokutana tena labda utaniambia ni mnyama gani anayekimbia kwa kasi zaidi duniani. Mimi pia nitajaribu kutafuta jina lake.

**Muziki**

## Sura ya 2: Nyumbani kwa Jack

---

**Jack:** Habari. Sasa niambie. Ni mnyama gani anayestahili nishani ya dhahabu kwa kukimbia kasi mita mia moja?

**Jenny:** Utafiti niliofanya katika mtandao wa internet ni kwamba mnyama anayekimbia kwa kasi zaidi duninani ni chui. Unajua kasi yake?

**Jack:** *(akifikiria):* Aah…. Labda kilomita 75 kwa saa?

**Jenny:** Umekosea mbali sana, Jack. Chui anaweza kukimbia kilomita 113 kwa saa, na humchukua sekunde tatu tu kufikia kasi hiyo. Waweza kuamini?

**Jack:** Kwa hivyo chui anaweza kupata kasi haraka hata kuliko gari?

**Jenny:** Kabisa!Lakini chui hawezi kudumisha kasi hii kwa muda mrefu. Anaweza tu kukimbia kasi hiyo kwa muda mfupi sana. Humsaidia anapokuwa mawindoni kwani huweza kumvamia mnyama anayemuwinda haraka sana. Lakini atashindwa na gari ikiwa ni mwendo mrefu. Hata lile gari kuu kuu zaidi pia litamshinda.

**Jack:** Jenny, nimegundua mnyama mwengine aliye na kasi zaidi kuliko chui. Kwa kweli angelimshinda angekuwa mkubwa kama chui.

**Jenny:** Kweli?  Nimnyama gani, huyobasi?

**Jack:** Anaitwa mjusi mpambe.

**Jenny:** Sijawahi kumsikia mnyam,a huyo.

**Jack:** Mjusi mpambe huishi katika nyika na majngwa ya Amerika. Ukubwa wao ni kama mkono wangu na wana mikia mirefu na miguu yao ya nyuma huwa na  guvu sana ambayo hutumia kutoroka adui.

**Jenny:** Kwa hivyo mjusi huyu hukimbia kwa kasi gani……. Aitwaje vile?

**Jack:** Anaitwa mjusi mpambe! Kwa kweli hana kasi ya chui yu mdogo sana na miguu mifupi. Kama mjusi mpambe angelikuwa mkubwa kama chui, angeliweza kukimbia  mita mia  moja kwa sekunde  0.83, amini usiamini! Ilhali chui ni sekunde 2.17.

**Jenny:** Ndio lakini  huyo mjusi wako ni mdogo sana hivi kwamba hastahili kuwekwa kwenye hesabu, kwa hivyo nimekushinda.

**Jack:** Tukubaliane ?

**Jenny:** Ndio, kwa sababu wewe hupendi kushindwa.Sasa tukubaliane nini?.

Jack: Kwamba wanyama wote wawili wanaweza kupata nishani za dhahabu-kulingana na  viwango vyao.

**Jenny:** Sawa, kwa kuwa umesema, hewala….. Lakini hebu tufikirie jambo lingine. Ni mnyama gani aliye na nguvu zaidi duniani.

**Jack:** Wazo zuri, lakini hebu nilifikirie nikiwa mazoezini kunyanyua uzani.

**Jenny:** Ati? Kunyanyua uzani. Uzani wa aina gani?.

**Jack:** Nafanya mazoezi ya kunyanyua uzani wa matangi ya maji. *( sauti ya matangi ya maji yakigongana)*

**Jenny:** Nidhani nitaweza kukutambua nikikuona baada ya kujenga misulu yako hiyo.

---

Scene 3: Jenny akutana na Jack katika uwanja wa michezo.

---

***Nyuma tunasikia sauti za watu wakifanya michezo mbali mbali.***

**Jack:** Jenny, Siamini!.

**Jenny:** Ni vyema  kukupata hapakwa uwanja wa michezo. Nisiamini nini?

**Jack:** Nimegundua kwamba mnyama mwenye nguvu zaidi ulimwenguni ni mdudu aina ya Kidundu yaani *(beetle).*

**Jenny:** *(kwa mshangao):*  Kidundu? *(Beetle?)*

**Jack:** Ndio kidundu  na hasa yule kifaru wa Ulaya.

**Jenny:** Aha. Kwani  Kidundu huyo ana nguvu kiasi gani

**Jack:** Kidundu kifaru ni kutoka jamii ya Kidundu wakubwa, na ana urefu wa kama kidole changu cha mwisho.Sikiliza kwa makini--  ana uzito wa gramu tatui tu lakini anaweza kubeba uzito mara 850 ya uzito wake. Lau kama angalikuwa kama binadamu, angaliweza kubeba  kilo elfu-54—na huo ni uzito wa kama magari makubwa 30. Lakini kwa kweli ndovu ndiye mnyama mwenye nguvu zaidi duniani!

**Jenny:** Kila ara ni …. lau kama!. Unazungumzia mnyama  ambaye  nguvu zake ni ikilinganishwa na ukubwa wake. Lakini ni wazi kwamba ndovu ndiye mnyama mwenye nguvu zaidi duniani!

**Jack:** Hiyo ni kweli—kama ungeweza kuwakutanisha katika mashindano ya mieleka wanyama hao wawili, bila shaka ndovu atashinda.

**Jenny:** Kabisa! Na sijali  kidundu kifaru huyo anaweza kubeba magari mangapi kama angelikuwa mkubwa. Mnyama wa pekee  anayeweza kunisaidia ikiwa gari langu litaingia mtaroni ni ndovu. Ndovu ana nguvu

sana hivi kwamba  ataweza kutumia mkonga wake kulitoa gari langu kutoka mtaroni.

**Jack:** Kwa hivyo ndovu anashinda nishani ya dhahabu kwa sababu ya kuwa na pua yenye nguvu zaidi!

**Jenny:** Na pia masikio makubwa zaidi!

**Jack:** Lakini ikija mambo ya kuruka umbali, ndovu hafai.

**Jenny:** Kwa nini  umefikiria kuhusu kurukja umbali.

**Jack:** Kwa sababu sasa nafanya mazoezi ya kuruka umbali.

**Jenny:** Kweli, nilikuwa nimesahau. Sijui ari hii ya uana-michezo itakuondoka lini?

**Jack:**Tosha kwa sasa kwani wapaswa kuwa na wakati wa kutafuta ni mnyama gani anayestahili nishani ya dhahabu kwa kuruka umbali mrefu?

**Jenny:** Hilo ni  mboga.

Muziki…..

---

## SURA 4: Baada ya shule, Jenny akutana na Jack barabarani

---

*Nyuma: Sauti za barabarani.*

**Jack:** Vipi Jenny? Shule ilikuwaje leo? Tuandamana kwenda nyumbani?

**Jenny:** Sawa

**Jack:** Je, ulipata kujua ni mnyama gani anayweza kuruka umbali mrefu?

**Jenny:** Ndio nimejua. Hivi punde tu nilimuuliza mwalimu wangu wa baiolojia. Mnyama huyo ni kangaroo. Na ni yule kangaroo mwekundu tu.

Wanyama hawa hupatikana Australia pekee. Wanaweza kuruka hadi umbali wa mita 13-unusu na urefu wa hadi mita 3.10 katika mruko mmoja tu.

**Jack:** Hiyo si mbaya. Inaonekana kana kwamba wanyama hao wana springi kwenye miguu yao.

**Jenny:** La hasha- hutumia miguu yao ya nyuma kuruka na ktumia mikia yao mirefu kulekea kule wanakotaka kwenda.

**Jack:** Alaa kumbe!.

**Jenny:** Kwa hivyo tunakubaliana kwamba kangaroo mwekundu ndiye anayestahili nishani ya dhahabu kwa kuruka umbali?

**Jack:** Ndio na la. Inategemea ukubwa wa mnyama. Nimefikiria mnyama mwingine—kama angelikuwa mkubwa kama kangaroo angemshindia mbali sana katika urukaji.

**Jenny:** Nilijua tu!

**Jack:** Nini?

**Jenny:** Nilijua utanitajia ka-mnyama ambako hakuna mtu anayekajua…

**Jack:** Ingawaje ni mdogo, lakini si mdogo hivyo. Nazungumzia nzige wa jangwani
Huyo ndiye anayestahili nishani ya dhahabu!

**Jenny:** Oooh. Kwani nzige wa jangwani anaweza kuruka umbali gani?

**Jack:** Anaweza kuruka mita mbili—umbali huo ni mara 30 urefu wa mwili wake. Kangaroo mwekundu ana urefu wa mita 1.6 hivyo basi atahitaji kuruka mita 52 kuweza kushindana na nzige huyo.

**Jenny:** Na wewe je, Jack, unaweza kuruka umbali gani?

**Jack:** Zaidi kidogo ya mita nne…

**Jenny:** Oooh! Rekodi ya dunia ni mita 8.95.

**Jack:** Kwa hivyo?

**Jenny:** Namaanisha ikiwa wataka kupata nishani ya dhahabu, basi yafaa uimarishe mazoezi yako.

**Jack:** Unajua, ukweli ni kwamba nilikuwa nimefikiria kwenda nyumbani. Nahisi uchungu kwenye mifupa na misuli yangu. Nahitaji kupumzika.

**Jenny:** Ala? Kwa muda gani!.

**Jack:** Kwa angalau miaka mitatu. Kwa sasa nadhani nimefanya riadha ya kutosha.

**Jenny:** Kwa kweli nafurahia kwamba umerudia hali yako ya kawaida.*( akimgonga gonga begani)* Sasa sijui nikupe nishani ya dhahabu kwa kujifanya mjuaji au kwa uzembe!

**Jack:** Uamuzi wako. Nishani ya dhahabu ninayokupa ni kwa kuwa rafiki yamgu mtundu zaidi.

## Muziki – Mwisho.

Outro

Sasa Jack amerudia hali yake ya kawaida na bila shaka shindano lijalo la ujuzi li karibu kuanza. Lakini ni hayo tu kwa leo kutoka kipindi chetu cha “ Tega sikio ujifunze” “Elimu ya Kawaida” kilichoandikwa na Leona Frommelt. Pia unaweza kutusikiliza kupitia mtandao wetu wa www.dw.de/kiswahili. Kwa sasa tunakushukuru na usisahau kututegea wakati ujao… kwaheri!